

**2023 Multicultural Community Grant Program
(Mpango wa Ruzuku ya Jumuiya za
Kitamaduni wa 2023): kutambua na kukabiliana na
Ukatili wa Nyumbani, Familia na Kingono**



Serikali ya NSW inatangaza Multicultural Community Grants Program (Mpango wa Ruzuku ya Jumuiya za Kitamaduni) juu ya Unyanyasaji wa Nyumbani, Familia na Kingono.

Jumla ya ufadhili wa \$2,000,000 unapatikana kwa ruzuku hizi za mara moja.

Waombaji waliofaulu wa ruzuku lazima wajenge uwezo wa jumuiya za tamaduni nyingi kutambua na kukabiliana na unyanyasaji wa nyumbani, familia na kingono.

Mashirika ya jumuiya ya NSW yasiyo ya faida yaliosajiriwa tu yanaweza kufanya maombi ya fedha hizi za ruzuku.

Ikiwa wewe ni shirika la jumuiya ya tamaduni nyingi ambalo halijasajiriwa, unaweza kushirikiana na shirika linalostahiki.

Ni lazima utimize miongozo madhubuti ya ruzuku ili kufanya maombi ya fedha kuanzia \$20,000 hadi \$150,000.

Maombi yanafunguliwa tarehe 13 Februari 2023 na kufungwa saa 11 jioni tarehe 27 Machi 2023.

Ili kujua zaidi kuhusu ruzuku hizi tembelea <https://www.dcj.nsw.gov.au/service-providers/grants/domestic-family-sexual-violence-multicultural-community-grant.html>

Iwapo unahitaji ushauri kuhusu mpango huu wa ruzuku, unaweza kuwasiliana na timu ya utoaji wa Ruzuku za Kitamaduni za DFSV kwa barua pepe kwa WFCS.DFSVMulticulturalGrant@facs.nsw.gov.au.

Serikali ya NSW inakaribisha ombi lako la ruzuku kwani unajua ni nini kitafanya kazi vyema kwa jamii yako.